

MANA ILIYO FICHWA

Ufunuo 2: 17:

Yeye aliye na sikio asikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa. Yeye ashindae nitampa baadhi ya ile manna iliyofichwa, nami nitampa Jiwe jeupe na juu ya jiwe hilo limeandikwa jina jipya asilolijua mtu Ila yeye anayelipokea.

Sikiliza kile nabii wa Mungu asemacho

Sasa, tukiwa na wazo hili akilini, tazama katika msitari tena. Nitampa manna iliyofichwa” Sote twajua kuwa manna ilikuwa ni chakula cha malaika, ilikuwa ndicho Mungu alichokishusha chini juu ya majani kwa Israeli katika wakati wao wa kuzunguka. Ilikuwa ni chakula kikamilifu (kutoka 16) ilikuwa inashangaza jinsi hizo chenga za chakula zilivyowafanya wadumu kuwa na afya kamilifu. Hakuna hata mmoja aliekuwa mgonjwa, ilikuwa ni yote waliyohitaji.

Wakati sanduku la agano lilipotengenezwa waliweka baadhi ya ile manna ndani yake kisha sanduku liliwekwa nyuma ya pazia na kuhani mkuu peke yake angethubutu kuingia na kisha ilibidi awe na damu ya matoleo.

Mkate toka mbinguni uliwakilishwa na manna, siku moja ulitoka mbinguni na ukawa uzima kwa wote waliomwamini Yeye. “Alisema Mimi ni mkate wa uzima. Mimi ni kate ulio hai utokao mbinguni mtu yeyote aulae mkate huu ataishi milele”. (Yoh 6:30 – 35, 48 – 58).

Nae alipoondoka, Yeye alituachia Neno lake, “Mtu hataishi kwa mkate tuu. Bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Bwana Mungu wako” (Math 4:4). Neno lake lilikuwa mkate. Ilikuwa ni manna kamilifu, ambayo mtu akiishi kwa hiyo,

hatakufa. Lakini mara baada ya vifo vya mababa, hakuna hata mmoja alieonekana kuwa anajua ile kweli hasa na kwa kitambo kidogo hii manna ilionekana kuwa inafichwa kwa watu. Lakini kila wakati Mungu alianza kurudisha ufunuo abao ulikuwa umefichwa mpaka wakati huu wa mwisho kulingana na ufunuo 10:7, Nabii atakuja na kufunua siri zote, na ndipo sasa Bwana atakuja.

Sasa katika kila wakati, nasema mjumbe hupokea kweli iliyofichwa. Lakini hawakuipokei wao binafsi tu. Lakini inakuwa kama ilivyokuwa kwa wanafunzi waliambiwa wagawie makutano mkate na samaki, Yesu aliwapa chakula kilichomegwa, nao waligeuka na kuwapa watu (Mark 6:30 – 44). Mungu huwapa manna iliyofichwa washindi. Haitakuwa kinyume chake. Hatafunguwa hazina yake kwa wale wanaokisukumia mbali kile ambacho tayari kimefunuliwa.

Kile nilichokuwa nikisema kuhusu mjumbe wa kila wakati akipokea toka kwa Mungu sehemu ya ukweli ule wa mwanzo wa Pentecoste ni mfano wa agano la kale wakati Musa alipoambiwa kutwaa vipimo vitatu na nusu vya manna na kuviweka katika chombo cha dhahabu nyuma ya pazia la patakatifu pa patakatifu (Kutoka 16: 33 – 34). Hapo kuhani mkuu wa kila kizazi angeingia na damu ya matoleo (waebrania 9: 5 -12). Kisha angechukua sehemu kidogo ya hii manna (kwa kuwa haiharibiki) ambayo ilikuwa ni sehemu ya ile ya asili na kuila. Sasa katika kila kizazi mjumbe wa Bwana wa kile kizazi hupewa ufunuo wa Mungu kwa ajili ya kile kizazi. Mara moja yule mjumbe anapoangaziwa na kweli, anaueneza ule ukweli kwa watu wote. Na wote ambao masikio yao yamefunguliwa na Yule Roho watasikia hiyo kweli, wataiamini, na kuishi kulingana na hiyo kweli.

Sasa, kuna wazo la kushiriki baadae ile manna iliyofichwa. Nafikiri itakuwa ni kushiriki milele ufunuo wa Yesu Kristo katika wakati wa umilele unaokuja. Ama isingewezekana

kuanza kujua utajiri usiochunguzika wa utu wake ? (Wakolosai 2: 2 -3; Waefeso 3:8).

Yale yote tuliyotamani kuyajua, maswali yetu yote yasiyokuwa na majibu, hayo yote yatafunuliwa. Kutoka kwa Kristo ambaye ni uzima wetu ambao tunaupokea. Oh, wakati mwingine tunawaza tunafikia kujua kidogo kumhusu Yeye, na Neno lake chini hapa, na ni vema sana, inatufanya sisi tufurahi; lakini siku moja wakati hu mwili takapobadilika, lile Neno na Yeye atakuwa kile hatukuwahi kuwa na ndoto kwamba ingewezekana kuwa.

Kwa hiyo malaika wa Mungu, Yule mjumbe kwa lile kanisa, anawajibika kama hatalihutubia lile Neno. Hiyo ni sawa. [1]

Manna iliyofichwa." Hebu tutowe tafsiri iliyo bora kadiri tutakavyoweza. Manna iliyofichwa inaeleza nini? Manna iliyofichwa ilikuwa ni manna iliyowekwa mahali au mkate wa uonyesha, katika biblia ambao ulikuwa kwa makuhani tu. (kut 25:30 ; Hesabu 4:1 – 8). Wangapi wanajua hilo ? unaona? Sasa haikuwa kwa... walikuwa na mkate kwa lile kusanyiko, na mkate maalum kwa kuhani. Hiyo ni sawa?

Huu ni mkate maalum. Mkate maalum manna iliyofuchwa ni kitu gani? Manna yetu ni nani? Kristo Yesu alisema alikuwa, ule mkate wa uzima utokao kwa Mungu toka mbinguni "ile manna.

Vema, manna iliyofichwa ni nini? Ni manna ile ambayo halipewi kusanyiko lote. Ufunuo unamiminwa kwa Yule malaika wa kanisa, ufunuo wa Neno, ufunuo wa Neno anapewa Yule malaika wa kile kizazi, kwa kuwa umefichwa mahali kote, na unafunuliwa tena (ile manna iliyofichwa) to anapewa malaika wa kile kizazi, kwa kuwa umefichwa mahali kote, na unafunuliwa tena (ile manna iliyofichwa) kwa .. Anapewa malaiko wa lile kansa unaona? Mmelipata hilo? Ni ufunuo mkubwa kidogo wa kile Kristo alichu, pengine ni wito wa juu kidogo, maalum. Ni nini? Sio kitu fulani cha ... zile Baraka za

Yule Roho Mtakatifu? Oh hapana, hizo ni kwa kundi zima. Lakini mana iliyofichwa ilikuwa ni ufumo maalum, sababu itabidi afundishe wengine unaona? Ujuzi zaidi kidogo wa maandiko, ili aweze kufundisha wengine. Anapaswa kufanya hivyo. Hiyo ni sawa? Hutaweza kuishi juu zaidi ya mchungaji wako. Wewe ukumbuke hilo unaona? Na kwa hiyo ..kwa sababu Yeye ni mchungaji, inabidi ajue manna ilipo, kulisha kondoo. Hiyo ni sawa? Sasa, maalum kidogo .. Na angalia hili kwa dakika tu, ule ufunuo, manna iliyo fichwa.

Na atakuwa na jiwe jeupe" (Ufunuo 2:17) hiyo ni sawa, " uadilifu."

Jina jipya, limeandikwa katika lili jiwe ambalo hakina alijuaye ila yeye mwenyewe" anajua yeye ni nani ila hawezi kuwaambia wengine. Unaona, unaona? Hakuna ajuaye ila yeye mwenyewe. Unaona? Petro alijua kuwa alikuwa na funguo, lakini hujawahi kumsikia akijisifu. Unaona? Hawa watu wanaojisifu kile walicho, kwa kawaida huwa hawana kitu, jiwe jeupe, na ndani yake jina jipya "sio jina lake mwenyewe, lakini yeye ni mtu mwingine na ni yeye mwenyewe anatambua (yeye alienalo lile jiwe, lile jina) unaona, manna maalum kulilisha kanisa , kumbuka [2]

Haileti tofauti yoyote kile watu wanasema. Unajua mwenyewe unapoingizwa ndani ya pazia la ndani. Hakuna awezaye kukuambia tofauti sio sababu umejiunga na kanisa, sababu umefanya hiki au kile, ila kitu fulani kinakuambia. Una jiwe ambalo liko moyoni, sio jiwe gumu, jiwe laini. Hili jiwe linafanya moyo wako laini badala ya kuwa mgumu [4]

Lilikuwa ni jiwe jeupe, ikimaanisha sio haki yake mwenyewe, bali haki ya Mungu mwenyewe [3]

Ndani ya Biblia, tunalipitia hilo, hapo katika nyakati za kanisa. Yesu ni manna iliyofichwa; Kristo ni manna ya kanisa. Manna

ni nini? Manna katika agano la kale kilichoshuka toka mbinguni, kipya kila usiku kulitia Kanisa nguvu katika safari yake. Hiyo ni sawa. Sasa katika agano jipya mana iliyofichwa ni nini? Bado kitambo kidogo ulimwnegu hautaniona tena (kufichwa), bali ninyi mtaniona mimi; kwa kuwa mtakuwa pamoja nami hata ndani yenu mpaka ukamilifu wa dhahari (Yoh 14:18 – 19). Na Kristo ni mana iliyofichwa itokayo kwa Mungu toka mbinguni kila siku.

Hatuwezi kusema, vema, wiki mbili zilizopita tulipata ujuzi wa Mungu. Vipi kuhusu sasa? Unaona? Kila siku mpya, Baraka mpya, kitu fulani kipya kinatoka kwa Mungu. Manna iliyofichwa inashuka toka kwa Mungu tokea huko mbinguni, Kristo. Na kinafanya karamu ya hii Manna ambayo ni Kristo, na Yeye analipa nguvu ya kuendelea na safari mpaka tuifikie ile nchi upande ule mwingine.

Manna iliyofichwa, jiwe, jina jipya ambalo hakuna alijuaye ila yeye mwenyewe. Na alilopewa Yule mjumbe wa kanisa. Nashangaa kama Luther alijua hili, nashangaa kama Wesley alilijua? Nashangaa kama malaika wengine wakuu ? [2]

Na sasa, tunakuta kiwa yeye pia alikuwa na manna iliyofichwa. Sasa, manna iliyofichwa ni mfano wa mkate wa uonyesho. Mikate ya uonyesho ilikuwa kwa kuhani peke yake. Hiyo ni sawa. Mkate wa uonyesho ulikuwa kwa ajili ya kuhani tu, ulikuwa umetengenezwa maalum kwa kuhani tu, huyo ni kiongozi, na huyu mtu ameshinda. kusanyiko lote lilopata manna, ila ana manna iliyofichwa maalum, au ufunuo maalum, oh, wa Yesu alichokuwa na ya kumhusu Yeye. Yote juu ya Yeye .Unaona? alipata ule ufunuo kama ameshinda. Kwa Yule malaika, “shikilia hilo kwa vile Ameshinda...” likimwambia Yule malaika wa kanisa .. unaona? [3]

Akitulisha na ile manna iliyofichwa ambayo wewe unasema tumepewa ndani ya ile Bibilia. Ambayo iliwekwa kwa ajili ya

makuhani tuu. Na tunafundishwa kuwa sisi ni makuhani wa Mungu, tukitoa sadaka za kiroho, ambayo ni, matunda ya midomo yetu, tukilisifu jina lake. (Petro 2: 9 – 10: Ufunuo 1: 5 – 6) [6]

Oh wakati Yeye alipomfufua Kristo toka kaburini, akikaa ndani yako, anahuisha miili yetu inayokufa kuingia katika uwepo wake. Wewe unatambua hili, wewe soi kunguru tena; wewe ni tai. Wewe kutaki yale mambo ya ulimwengu. Wewe ni mwana na binti wa Mungu. Uko kwenye karamu ya chemchem ambayo ulimwengu haujui kitu kuhusu, unakunywa kwa mtu fulani anajua ... ulimwengu haujui chochote juu yake, unakula manna iliyofichwa ambayo ulimwengu hauji chochote juu yake kwa kuwa wewe ni tai, unahuishwa mahali wewe unapoweza kuifikia. Huwezi kuipata hapa chini, inabidi upande juu hapa. Inabidi uhuishwe, uinuliwe juu pale, ili uhuishwe. [7]

Nukuu za kiingereza

[1] Wakati wa kanisa la perapima;Nya. saba uk. 210 – 211

[2] Wakati wa Kanisa la pergamo, (60 – 1207) aya 302 – 305, 312 – 313, 315 – 319)

[3] Wakati wa Kanisa la Thiatira (60 – 1208) aya 31, 35

[4] Kwa nini watu wanatupwa tupwa (56 – 0101) uk. 17

[5] Maswali na majibu” (61 – 1015m) aya 83 – 84

[6] Uinjilisti wakati wa mwisho (62 – 0603) aya ya 3

[7] Kuchomoza kwa jua (65 – 0418) aya 31.

Jiwe la kujengea la kiroho nambari 182 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa saa hii, yamekusanywa na Gerd rodewald friendstr. 69.D-75328 Schomberge Germany Simu (+49) 2357613 Fax 72353306.

Amekuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Bibilia na kazi ya haraka itazunguka dunia.

Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia (Ndugu Branham katika mwenendo, utaratibu na mafundisho uk724.)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili andika kwa:

Charles E. Y. Kanju,

Box 553 Korogwe - Tanga

E-mail: Chaelika@live1.com

Cellphone: 0784 704299/ 0713230098

